

MIPASHAHE.

Adui wa haki rushwa adhibitiwe, ni hasara kuzidi kupambana naye

Na Dk Reuben Lumbagala

RUSHWA ina majina mengi utasikia mlungula, kitu kidogo, hongo, chai, chauchau na wapo wanaosema kunjua mkono, laini mchakato na hata zunguka mbuyu.

Kwa ujumla tafsiri ya neno 'rushwa' haibadiliki ni ile ile kutoa fedha au kitu kingine cha thamani hata mwili wa mwanamke ili kupata upendeleo au haki unayoitaka.

Rushwa pia ina maana ya matumizi mabaya ya ofisi kwa maslahi binafsi ambayo leo hali hiyo imekuwa tatizo la kijamii na duniani ambako kila nchi inafanya jitihada zake katika kuipunguza au kuikomesha.

Tanzania si kisiwa, hivyo rushwa inaikabili pia nchi hii na ndiyo maana juhudi mbalimbali zinafanyika kuipunguza au kuimaliza, zikianzishwa taasisi za kuikabili mfano ya Kuzuiia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ya Usuluhishi wa Malalamiko ya Kodi



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene. **PICHA: MTANDAO**

Halikadhalika wananchi kukosa kabisa miradi ya maendeleo ambayo kama ingetekelezwa ipasavyo, ingeweza kuboresha hali za maisha yao na kuchochea maendeleo na ustawi wa wananchi mijini na vijijini.

Ni muda mwafaka sasa kuhakikisha kuwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kanuni na sheria zote zinazingatiwa ili kuondoa mianya ya rushwa.

Mathalani, upatikanaji wa mزابوني wa kutekeleza miradi ya maendeleo, apatikane kwa uwazi na akidhi vigezo vyote. Vilevile, hata baada ya kushinda zabuni hiyo, afuate sheria, taratibu na mifumo ya manunuzi kikamilifu katika kutekeleza miradi ili kazi ziakisi thamani ya fedha na wananchi wafurahie ujenzi au jambo linalofanyika.

Kama watendaji hawataziba nyufa kwa kutenda haki kwa wazabuni wanaotekeleza miradi ya maendeleo na kufuatilia ubora wa kazi, ni dhahiri watapatikana wasiokidhi vigezo na hivyo kufanyakazi chini ya viwango na

